

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



MWITO WA KUTOA MAONI

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

S/N	Jina la Mwombaji	Eneo	Jina la Mkurugenzi/Uraia	Aina ya Leseni
1.	Pmax Co. Ltd- Njombe Service Station S.L.P 637 Njombe	Kiwanja Na. 219, Kitalu "T", eneo la Nazareth, Njombe Mjini, Mkoa wa Njombe	Max Kanut Mlelwa (Mtanzania)	Leseni ya kituo cha mafuta
2.	Njombe Filling Station S.L.P 411 Njombe	Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Kijiji cha Lupembe, Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Njombe	James Malika Mwinuka (Mtanzania)	Leseni ya kituo cha mafuta
3.	Kapunga Rice Project Limited S.L.P 45	Kiwanja Na. 628/2, Kijiji cha Kapunga, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa	Antoneta Sebastian Fialho (Mtanzania)	Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi

S/N	Jina la Mwombaji	Eneo	Jina la Mkurugenzi/Uraia	Aina ya Leseni
	Chimala - Mbeya	Mbeya		
4.	SBC Tanzania Limited S.L.P 4162 Dar es salaam	Kiwanja Na. 54-57, Eneo la Kipawa, Wilaya ya Ilala, Dar es salaam	Ziad El Khalil (Raia wa Uingereza)	Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi
5.	Matemba Filling station S.L.P 141 Turiani	Eneo la Sungaji, Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro	Dickson Matemba (Mtanzania)	Leseni ya kituo cha mafuta
6.	Ahmed Abdallah Bakhamis S.L.P 20 Kilosa	Kiwanja Na. 1, Kitalu A, Eneo la Kibaoni, Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro	Ahmed Abdallah Bakhamis (Mtanzania)	Leseni ya kituo cha mafuta
7.	Landmark Filling Station Mvumi, S.L.P 64, Kongwa, Dodoma	Eneo la Mvumi, Kata ya Mvumi, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma	Fatuma Ramadhan Mganga (Mtanzania)	Leseni ya Kituo cha Mafuta
8.	Landmark Filling Station Hombolo, S.L.P 64, Kongwa, Dodoma	Eneo la Hombolo, Kata ya Hombolo, Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma	Fatuma Ramadhan Mganga (Mtanzania)	Leseni ya Kituo cha Mafuta
9.	Khalid Salum Said T/A Green Apple Filling Station S. L. P 80, Kigoma	Kiwanja Na 6MD, Kitalu A, Eneo la Mlote, Manispaa ya Kigoma- ujiji, Mkoa wa Kigoma	Khalid Salum Said (Mtanzania)	Leseni ya Kituo cha Mafuta

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

Imetolewa na:

**Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**